JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI

OFISI YA RAIS
TAWALAA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI KOROGWE

# MKATABA WA KUPANGISHA MAGHALA MAWILI (2) NA OFISI MBILI (2)

LGA/126/2020/2022/NC/08

KATI YA

HALMASHAURI YA MJI KOROGWE
S.L.P 615, KOROGWE

NA

Certified True Copy of the Original
Sign: ______ Date: 17.11.2020
FREDRICK K. FUNGAMTAMA
Advocate, Notary
Public & Commissioner for Oaths

M/S CYREKA EAST AFRICA DEVELOPMENT CO. LTD
S.L.P 5017 TANGA

## MKATABA WA KUPANGISHA MAGHALA MAWILI (2) NA OFISI MBILI (2)

Mkataba huu wa kupangisha Maghala mawili (2) na Ofisi Mbili (2) umetiwa saini leo tarehe **01** mwezi wa **07** mwaka **2020**

**KATI YA**

**HALMASHAURI YA MJI KOROGWE SLP**. 615 (ambaye katika mkataba huu ataitwa 'Halmashauri') kwa upande mmoja

**NA**

**M/S CYREKA EAST AFRICA DEVELOPMENT CO. LTD** wa S.L.P 5017 TANGA, TANZANIA (ambaye katika mkataba huu ataitwa "Mpangaji" neno litakalojumuisha wabia na warithi wake) kwa upande mwingine wa mkataba huu.

**KWA KUWA** Halmashauri inamiliki Maghala Mawili (2) pamoja na Ofisi Mbili (2) ambayo yamejengwa kwenye ardhi ambayo haijapimwa katika Mtaa wa KWAZOMOLO kata ya OLD KOROGWE, HALMASHAURI YA MJI KOROGWE iko radhi kuingia katika makubaliano na KAMPUNI YA CYREKA EAST AFRICA DEVELOPMENT CO.LTD kampuni ambayo inajihusisha na Biashara ya Mkonge juu ya upangishwaji, upangaji na ulipaji wa Kodi ya upangaji wa Maghala pamoja na Ofisi hizo,

Ufuatao ni ushuhuda wa makubaliano

1. Kwamba,Halmashauri itapokea kodi ya kupanga Maghala hayo pamoja ofisi yaliyopo katika Mtaa wa Kwazomolo, kata ya Old Korogwe katika Halmpashauri ya Mji korogwe
2. Kwamba mkataba huu utakuwa ni wa miaka miwili (2) na utaanza tarehe **01/07/2020** na kumalizika tarehe **30/06/2022**. Na baada ya muda huo Mmiliki ataamua endapo atahitaji kuendelea kupangisha majengo yake na hivyo utatolewa mkataba mwingine kutokana na wahusika watakavyo kubaliana.
3. Kwamba Mpangaji atatumia Maghala hayo pamoja na Ofisi hizo kufanyia biashara halali iliyokusudiwa kufanywa na si vinginevyo.
4. Kwamba pande zote zinatambua kuwa mpangaji ametumia gharama ya Tshs. 12,000,000 kufanya ukarabati wa maghala mawili (2), ofisi mbili (2) na Choo na ufidiaji wa gharama za ukarabati utafanyika kwa kukata sehemu ya malipo ya kila mwezi.

5. Kwamba kodi ya upangaji kwa mwezi ni shilingi **MILIONI MOJA NA LAKI MBILI (1,200,000/=) HIVYO** Mpangaji atatakiwa kulipa kiasi cha shilingi **MILIONI ISHIRINI NA NANE NA LAKI NANE (28,800,000/=)** kama kodi ya kupangishaji Maghala hayo pamoja na Ofisi kwa miaka miwili (2)
6. Kwamba utaratibu ni kutoa kiasi cha shilingi **MILIONI SABA NA LAKI MBILI (7,200,000/=)**kwa miezi sita. Kiasi cha Shilingi **MILIONI NNE NA LAKI MBILI (4,200,000/=)** kitalipwa kwa Halmashauri na kiasi cha shilingi **MILIONI TATU (3,000,000/=)** kitakuwa ni kwa ajili ya kufidia gharama za ukarabati.
7. Kwamba utaratibu wa malipo utakuwa kama ifuatavyo:-
    a) Malipo ya kwanza yatakuwa ya miezi 6 kuazia Julai – Desemba, 2020 yatalipwa kabla ya kusaini Mkataba.
    b) Malipo ya pili yatakuwa Januari- June, 2021 na yatalipwa Januari, 2021.
    c) Malipo ya tatu yatakuwa Julai- Desemba, 2021 na yatalipwa Julai, 2021
    d) Malipo ya nne yatakuwa Januari- Juni, 2022 na yatalipwa Januari, 2022.

Pia inasisitizwa katika makubaliano haya kuwa muda na kiasi cha malipo uzingatiwe ili kuepusha migogoro baina ya pande zote mbili za mkataba.

8. Kwamba,mara baada ya kusaini mkataba huu, Mpangaji atatakiwa kuanza kufanya biashara ndani ya muda wa siku saba tokea kusaini mkataba.
9. Kwamba Mpangaji hataruhusiwa kufanya biashara mpaka awe amelipa kiasi tajwa cha makubaliano siku ya kusainiwa kwa mkataba.
10. Kwamba, Halmashauri itakuwa huru kuvunja mkataba huu muda wowote itakapobaini kuwa masharti yaliyopo katika mkataba huu yamevunjwa au yanakaribia kuvunjwa na Mpangaji atalazimika kulipa hasara yote ambayo itapatikana kutokana na uvunjwaji huo.
11. Kwamba ,Halmashauri pamoja na Mpangaji watakuwa huru kuvunja mkataba huu kabla ya muda wa mkataba kuisha endapo mmojawapo atatoa taarifa ya siku tisini (90) juu ya nia yake ya kutaka kuvunja mkataba.
12. Kwamba,Mpangaji atatakiwa kufanya usafi na kutunza Mazingira kwa kuzingatia Mpango wa utunzaji Mazingira ( EPP) ambao amesha utia saini.
13. Kwamba Mpangaji atairuhusu kwa wakati muafaka Halmashauri kuingia,kukagua Maghala hayo pamoja na Ofisi
14. Kwamba,litakuwa jukumu la Mpangaji kulipia gharama zote za Maji na umeme zitakazotumika katika Maghala hayo pamoja na Ofisi.
15. Kwamba, mawasiliano yote yanayohusu mkataba huu yatafanyika kwa njia ya maandishi na si vinginevyo.
16. Kwamba, a) pande zote zitajitahidi kusuluhisha mgogoro huo kwa njia ya majadiliano

    b) Kama mazungumzo yatashindwa kuleta makubaliano,basi mgogoro utasuluhishwa kwa muijibu wa ***Sheria ya Usuluhishi wa Migogoro,***

***sura ya 15 ya Sheria za Tanzania.( The Arbitration Act, Cap 15 R.E 2002***) na Msuluhishi atakuwa Katibu Tawala Wilaya (DAS).

**KWA USHAHIDI WA MAKUBALIANO** yaliyotajwa hapo juu PANDE ZOTE MBILI zimetia saini kama inavyooneshwa hapo chini:-

**UMETIWA SAINI NA;**

**KWA UPANDE WA HALMASHAURI**

TOWN DIRECTOR
KOROGWE TOWN COUNCIL
KOROGWE

JINA: **NICODEMUS J. BEI**
TAREHE ____________________

MKURUGENZI
HALMASHARI YA MJI
KOROGWE

**KWA UPANDE WA MPANGAJI**

JINA THOMAS M. TARUMBETA
CHEO H.R
SAHIHI
TAREHE 08/04/2020

CYREKA AFRICA EQUIPMENT COMPANY LIMITED TANZANIA

Certified True Copy of the Original
Sign: Date: 17.11.2020
FREDRICK K. FUNGAMTAMA
Advocate, Notary
Public & Commissioner for Oaths